

Uzinduzi wa mkakati kitaifa wa Kilimo Ikolojia-hai (NEOAS)



Mkulima Mbunifu, ilipata fursa ya kuhudhuria Mkutano wa tatu wa kitaifa wa kilimo ikolojia-hai uliofanyika Novemba 8 hadi 9 jijini Dodoma, chini ya uratibu wa mwavuli wa Taasisi za kilimo hai Tanzania (TOAM), kwa kushirikiana na wizara ya Kilimo Tanzania. Mkutano huu ulitoa fursa ya kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Ikolojia-Hai (NEOAS) unaolenga kuweka mikakati ya kuimarisha kilimohai nchini Tanzania.

Daudi Manongi

Mkutano huo ukiwa na kaulimbiu ya Tunza Asili, kwa Afya Bora ulilenga kuchochea utekelezaji kwa vitendo jitihada mbalimbali zilizopo kwa ajili ya kukuza sekta ya kilimo ikolojia-hai, ambapo ulikutanisha wadau mbalimbali katika sekta ya kilimo.

Ifahamike kuwa kilimo ikolojia ni muhimu kwa watanzania kwani mazao yake ni muhimu katika kuleta tija kiuchumi, lakini pia kulinda afya za walaji, afya ya udongo na kuongeza kipato kupitia bidhaa zinazozaliashwa hivyo kuwa na kilimo endelevu.

Mkakati huu unaotarajiwa kutekeleza kwa miaka 7 kuanzia mwaka 2023 mpaka mwaka 2030, unalenga kuleta masuluhi na hivyo kuleta tija katika sekta ya kilimo. Miongoni mwa masuluhi kupitia mikakati mahususi ni katika maeneo yafuatayo,

- Utafiti kwa teknolojia na mbinu za kilimo hai zeny kuleta tija katika uzalishaji, uhifadhi na kuongeza thamani.

Kwa uhitaji wa jarida hili wasiliana nasi kwa kutupigia simu au kwa anwani kwa kupitia barua pepe, facebook, tovuti na sanduku la posta kama zilivoonyeshwa hapa;

- Kusambaza elimu na teknolojia za kilimo hai kwa wakulima na wadau wa mnyororo wa thamani.
- Kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbegu, kurutubisha udongo na kukabiliana na magonjwa kwa njia endelevu na zilizo na uendelevu kwa afya ya udongo na walaji.
- Kuhakikisha wa wakulima wanathibitishwa na kufikia masoko ya kilimo ikolojia hai.
- Kusambaza elimu kwa walaji kuhusu faida za kutumia bidhaa za kilimo ikolojia hai kwa uedelevu na afya za udongo na afya zao.
- Kutatua changamoto za masuala ya kujinsia hivyo kuhakikisha sekta ya kilimo haiachi wanawake na vijana nyuma.

Mkakati kwa ujumla unatoa taswira nzima itakayoleta ufanisi wa Kilimo Ikolojia na kilimo kwa ujumla nchini.

Mkurugenzi mtendaji wa shirika la Biovision African Trust (BVAT), Dkt. David Amudavi alishiriki katika mkutano huu, ambapo amesema kilimo ikolojia-hai ni maisha pia ni chakula na wanahitaji kuona Afrika ikiwa mahali salama na watu wanaishi maisha na mazingira ya afya nzuri kupitia kilimo cha ikolojia.

Aliendelea na kusema Kilimo hai kimepewa kipaumbele na viongozi wetu wa nchi zote za Afrika. Mwaka wa 2010 mawaziri wote wa kilimo Afrika walithibitisha sheria iliyoainisha kwamba kilimo hai kipatiwe nafasi katika nchi zetu zote za Afrika na mwezi January 2030 viongozi wataweka sahihi.

Yaliyomo

Kutengeneza chakula cha mifugo	2
Tumia mvua kwa faida ya baadaye	6



Faida za tangawizi ya embe	9
Mshirika wa Mkulima Mbunifu	11

Mpendwa Mkulima

Tumefikia mwezi wa mwisho katika mwaka huu wa 2023. Kwa kawaida mwezi huu, huwa na shamrashamra za aina mbalimbali ambazo huandamana na gharama kubwa kwa ajili ya kukamilisha pilikapilkila hizo.

Jambo hili ni nzuri kwa kuwa ni furaha kwa ajili ya yale ambayo uliweza kuyafanya kuanzia mwanzoni mwa mwaka hadi kufikia mwisho, halikadhalika kushukuru kuweza kufika mwishoni mwa mwaka.

Pamoja na hayo yote, ni muhimu sana kufikiria na kukumbuka kuwa mwisho wa mwezi huu ni mwanzo wa safari nyingine mpya inayokuwa na changamoto nyingi inapoanza. Endapo utakosea tu mwanzoni mwa safari hiyo mpya, basi ujue kuwa safari yote kwa kipindi cha miezi kumi na mbili inayofuata itakuwa ngumu sana.

Kwa mwaka mzima jarida hili limetoea elimu kwa kiasi kikubwa kuhusiana na utunzaji wa mazingira pamoja na utekelezaji wa shughuli za kilimo na ufugaji kwa misingi ya kilimo hai.

Hima mkulima! Weka mikakati sawa kwa ajili ya uzalishaji kwa mwaka 2024. Hii ni pamoja na kuandaa shamba, mbegu, na pia kuweka mipango sawia juu ya uvunaji na uhifadhi wa mazao.

Mkulima Mbunifu inasilitiza matumizi ya mbolea za asili, dawa za asili na kufuata misingi ya kilimo hai.

Kwa niaba ya Shirika la Biovision Africa Trust (BVAT), Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), wafanyakazi wa Mkulima Mbunifu, wafadhili wa jarida la Mkulima Mbunifu - Biovision Foundation, tungependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa wadau wote kwa ushirikiano wenu. Tunawatachia heri ya sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya wa 2024.

Namna ya kutengeneza chakula cha mifugo (silage)

Aina ya chakula hiki ni kizuri sana kwa ng'ombe wa maziwa, matokeo ya ongezeko la maziwa yataonekana kwa muda mfupi sana.

Irene Mark

Pia chakula hiki huweza kupewa wanyama wengine kama kondoo, mbuzi, nguruwe n.k

Mahitaji:

- Majani mabichi(nyasi au mazao ya nafaka)
- Molases
- Maji
- Mfuko wa plastic(polythene bags), mapipa au shimo
- Panga au mashine ya kukatia majani(chaff cutter).

HATUA ZA KUTENGENEZA SILAGE

Majani yakatwe na kuachwa kwa angalau siku moja ili kupunguza kiasi cha maji, ni vizuri kwa mazao ya nafaka kuvunwa wakati yametoo mazao tayari ili kuongeza ladha na virutubisho.

1. kata majani kutumia panga au mashine katika urefu wa inch 1(2.5cm).
2. Tandaza chini karatasi la plastic au turubali.



Mkulima Mbunifu ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradhi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelizwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

3. Pima majani yaliyo katwa kiasi cha kilo 50-70 na uweke kwenye karatasi ulilotandaza.
4. Pima lita 1 ya molases na changanya na maji kiasi cha lita 1 hadi 3.
5. Nyunyiza mchanganyiko(molases na maji) katika majani ulio yapima kiasi cha kilo 50-70, hakikisha sehemu zote zinapata molases kwa kuyageuzeza.
6. Rudia hatua ya 1 hadi 5 hadi upate kiasi cha kukutosha.
7. Kama unatumia shimo, utachimba shimo la kuweka karatasi ya nayloni(polythene sheets) ili majani yasigusane na udongo. Pia unaweza kutumia mapipa ya plastic au mifuko ya nylon.
8. Chukua mchanganyiko wa majani na molases kisha hifadhi kwenye mapipa au mifuko ya plastic au kwenye shimo ulilo andaa, weka kwa kushindilia ili kuondoa hewa.
9. Ukiisha weka kwenye chombo cha kuhifadhiya kama pipa, mifuko ya plastic au shimo, funga kwa kukaza kuhakikisha hewa haingii ndani ili kuzuia kuoza.
10. shimo, hakikisha unafunika kwa karatasi ya nayloni na kuweka vitu vizito juu.
11. Hifadhi mbali na jua au mvua,
12. Baada ya siku 30 hadi 40 chakula kitakuwa tayari kulisha mifugo yako.



ZINGATIA

- *Hakikisha maji na hewa haingii ndani ya chakula chako wakati wa kuhifadhi.*
- *Utakapo fungua toa kiasi cha kulisha kwa muda huo na kingine endelea kufungia na kuzuia hewa kuingia.*
- *Wanyama wa maziwa wapewe angalau masaa 3 kabla ya kukamua kuepusha harufu katika maziwa.*
- *Silage nzuri itakuwa na kijani na rangi ya ugoro(greenish brown).*

Mpangilio: Cathbert Msemo 0652 731 123

Mhariri: Erica Rugabandana

Mhariri Msaidizi: Flora Laanyuni

Anuani: *Mkulima Mbunifu*

Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)

S.L.P 14402, Arusha, Tanzania

Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366

Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876

Barua pepe: info@mkulimambunifu.org

www.mkulimambunifu.org



Wachapishaji: African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

Jihadhari na sumukuvu kwa kuhifadhi mazao kwa usalama

Utafiti uliofanywa na wataalamu mbalimbali wakiwepo wataalamu kutoka Taasisi ya utafiti wa Kilimo ya Seliani (SARI) wamebaini kuwa, sumukuvu (Aflatoxin) inayotokana na fangasi, husababisha ugonjwa wa saratani ya ini kwa binadamu na wanyama. Utafiti huo pia uneleza kuwa, ugonjwa huo unaweza usionekane kwa haraka na huweza hata kuchukua muda wa mwaka ndipo ujitekeze.

Atanas Masao

Watu wengi hawana ufahamu mzuri juu ya sumu hii ambayo haionekani kwa macho hivyo hawazingati kanuni bora za kilimo, uvunaji na ukaushaji sahihi, utunzaji salama, usafirishaji hatarishi na usindikaji mbaya. Lakini mabadiliko ya tabianchi yamechangia kuweka mazingira rafiki kwa fangasi wabaya kuongezeka kwa urahisi.

Sumukuvu ni nini?

Ni sumu ambazo huzalishwa na fangasi wanaoshambulia mazao shambani au ambayo hayajakauka vizuri. Sumu hii ikishaingia kwenye mazao ni vigumu kuitoa, iwe kwa kupika au kukaanda

Kwanini tushughulikie sumukuvu kwa sasa?

Sumu hii huleta athari kwenye usalama wa chakula, afya na biashara.

Kwa namna gani?

1. Katika kiwango kikubwa sumukuvu inaweza kupelekea vifo vya watu na wanyama. Ni mojawapo ya kisababishi kikubwa cha saratani ya ini na koo.



Picha:IN

- 2. Katika watoto sumukuvu inasababisha udumavu na kuathiri ukuaji. Aidha sumukuvu hodhoofisha kinga ya mwili na kupelekea kupatwa na magonjwa mengine
- 3. Sumu hii yaweza kuua wanyama endapo itakua katika kiwango kikubwa na hupunguza tija katika uzalishaji mayai, nyama au maziwa
- 4. Huathiri biashara, jamii na uchumi kwani hatutaweza kuuza mazao yetu katika masoko ya ndani na nje hivyo kukosa kipato

Mazao gani huathiriwa zaidi na sumukuvu?

Mazao ambayo huathiriwa zaidi hasa yanapokaushwa vibaya shambani ni;

- Nafaka: mahindi, mtama na uwele
- Mikunde: karanga, soya
- Mbegu za mafuta: alizeti
- Viungo: pilipili zilizokaushwa
- Mazao yaliyosindikwa: unga wa mahindi, siagi ya karanga, chakula cha mifugo, mihogo
- Mazao ya mifugo: maziwa na mazao yake, mayai au nyama kutoka kwa mnyama aliye kula chakula chenye sumukuvu

Mambo ya kuzingatia ili kuzuia sumukuvu

- Karabati, safisha na tumia viuatilifu

Picha:IN

- katika ghala au chumba cha kuhifadhiya mazao
- Weka mazao yaliyokauka vizuri kwenye vifaa vya kuhifadhiya kama mifuko isiyongiza hewa vihenge vya chuma au plastiki na magunia
- Weka mazao yako juu ya paleti, mbaou au miti hakikisha kuna nafasi angalau mita moja kutoka ukutani wakati wa kuhifadhi ili kuruhusu mzunguko wa hewa
- Zuiwadudu na panya kwa kutumia viuatilifu vilivyopendekezwa wakati wa kuhifadhi ghalani
- Kagua mazao yako mara kwa mara kuhakikisha hakuna mashambulizi na kausha tena mazao yako inapobidi

Mambo ya kuepuka ili kuzuia sumukuvu

- Usirundike mazao yako kwenye ghala bila kua na mzunguko mzuri wa hewa
- Usirundike mazao ambayo hayajawekwa kwenye vifungashio kwenye ghala hasa mahindi kwani hupelekea uchafuzi wa sumukuvu
- Usichanganye mazao ya zamani na mapya kwani inaweza kuwa chanzo cha mashambulizi ya fangasi wa sumukuvu
- Usihifadhi nafaka kwenye magunia au viroba vilivyotoboka

Itumie mvua vizuri kwa faida ya baadae

Msemo wa siku ya chakula duniani 2023 "Maji ni uhai, maji ni chakula"
Usemu huu ni kweli na hakika kwani bila maji Maisha ya binadamu na wanyama huwa magumu sana. Mimea hutegemea maji na binadamu na Wanyama hutegemea pia mimea.

Erica Rugabandana

Mabilioni ya lita za ujazo za maji humwagika chini wakati wa mvua, kulingana na kupungua kwa vyano vya maji, wakulima ni lazima wavune na kkusanya kiasi kikubwa cha maji watakachowea, ili kuyatumia wakati wa kiangazi. vyano vya maji vilivyopo, na namna ambayo maji yataweza kuvunwa, na kuhifadhi na lazima vizingatiwe. Hii ni sawa na vile ambavyo unavuna mazao ambayo yanaipatia familia yako chakula cha kutosha mwaka mzima, maji ni lazima pia yawepo kwa ajili ya familia, wanyama na mashamba kwa muda wote wa kipindi cha kiangazi.

Unahitaji kuhifadhi maji kiasi gani?

Kwa makadirio ya kawaida, jedwali hilo hapo chini linaweza kutumika. Kiasi kikubwa cha maji kinahitajika endapo mazao ni ya kumwagilia. Kwa kuzingatia kiasi cha maji, ng'ombe wa maziwa pia wanatakiwa kuhesabiwa.

Makadirio ya maji yanayohitajika shambani	Lita kwa siku
Mtu 1	15
Ng'ombe 1 wa maziwa kulingana na kiasi cha maziwa anachozalisha na malisho	50 – 80
Ng'ombe 1 wa kienyeji	35
Mbuzi 1 au kondoo 1	2 – 5
Kuku 1	0.25
Ekari 1 inayonyeshewa kwa matone (skwea mita 400;3.3mm)	13,200
Ekari 1 inayonyeshewa kwa mifereji (5 mm)	20,000

Mfano: nyumba yenyne watu 6, ng'ombe 1 wa maziwa, mbuzi 4 na kuku 20 wanahitaji kiasi cha lita 21,000 wakati wa kiangazi kwa kipindi cha miezi 4. Ng'ombe wa maziwa atatumia moja ya tatu ya kiasi hicho

Kama robo moja itanyeshewa kwa matone katiak siku 60 za kiangazi, kiasi cha lita 200,000 zaidi za maji zinahitajika ni lazima zihifadhiwe.

Maji ya paa ni safi kwa matumizi ya nyumbani

Vuna maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo, na maji ambayo sio lazima yaye safi kwa ajili ya mazao. Chanzo kizuri cha maji safi ni maji ya mvua. Mabati yanaweza kusaidia kukusanya maji safi katika kipindi chote kwa mwaka. Kinachohotajika ni kutengenezea mabomba na kuyaelekeza kwenye matanki ya kuhifadhi.

Tumia mapaa yote yaliyopo kwenye eneo lako kuvuna maji ya mvua. Pia maji yanayotoka kwenye mapaa madogo kama vile mabanda ya mifugo yanaweza kuvunwa na kuhifadhi kwenye matanki madogo madogo. Nyumba yenyne familia ya watu 6 hutumia lita 100 za maji kwa siku. Kwa mwaka mzima ujazo wa mche mraba(cubic)36 za maji zinahitajika. Kwa sehemu ambazo si kame sana (zinapata mvua kiasi cha milimita 600 kwa mwaka) kiasi hiki cha maji kinaweza kuvunwa kutoka kwenye paa lenye mita mraba 60. Hii inalingana na nyumba yenyne ukubwa wa mita 6 x mita 10.

Matanki ya kuhifadhi

Matanki na mapipa ama vifaa vinginevyo vya kuhifadhi maji kuchafuliwa.

Kwenye mteremko, bwawa ni lazima liwe umbo la mviringo au yai, ili kuzuia nguvu ya maji yanayoingia kwenye bwawa ama kutoka kusababisha mashimo kwenye kuta. Unaweza kutengeneza kwa kutumia udongo wa mfinyanzi ili kufanya sakafu ya bwawa kuwa imara. Kwenye sehemu zenyne mwinuko, bwawa la umbo nusu duara linafaa zaidi kwa kuhifadhi maji. Unaweza kujenga mfereji kwa kutumia mawe ili kupunguza maji yanayozidi kwenye bwawa. Kutoka kwenye bwawa mifereji midogo ya kuchuja maji yanayotoka bwawani kwenda shambani hutengenezwa.

Ongeza bwawa lako taratibu

Mkulima anaweza kuanza kwa kuchimba bwawa dogo wakati wa kiangazi na kuliongeza kila mwaka, mpaka hapo atakaporidhika na ukubwa wa bwawa.



Je, njia za asili za kukabili wadudu na magonjwa ni zipi?

Viumbe wajulikanao kama wadudu au vijidudu wanaosababisha magonjwa hutambulika kutokana na madhara wanayoleta kwenye mimea. Iwapo mandhari hayataku na uwiano basi sehemu moja inaweza kuwa na idadi kubwa ya wadudu waharibifu hivyo kusababisha madhara.

Eliudi Letungaa

Madhumuni ya njia hizi za asili ni kujaribu kuweka uwiano katika mazingira. Mfumo huu haukusudii kuangamiza wadudu bali kuwakabili.

Ni bora basi kuchukua tahadhari na kuzuia mimea isishambuliwe ili kudhibiti hasara inayoweza kupatikana iwapo mimea itashambuliwa (sio mazao hafifu, bali pia gherama kubwa ya madawa)

Je, kutumia njia za kiasili ni bora kuliko madawa ya kemikali?

Madawa ya kemikali hayaleta suluhisho na ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la magonjwa na wadudu katika mazingira. Matumizi ya kemikali yameongezeka zaidi kipindi cha miaka 50 iliyopita ilihali idadi ya magonjwa na wadudu imezidi kuongezeka na wengine kuweka usugu hivyo kutoangamizwa na kemikali hizo. Wakati mwengine madawa ya kemikali yamesababisha madhara kwa watumiaji, mazingira na hata walaji hali iliyosababisha matumizi ya baadhi ya kemikali kupigwa marufuku na pia kuweka viwango vya kudhibiti ubora na usalama wa chakula.

Zifuatazo ni faida zinazothibitisha umuhimu wa njia za kiasili

Gherama

Gherama ni kidogo ukilinganisha na madawa ya kemikali. Kwani vitu vinavyotumika kutengeneza madawa ya asili hupatikana kwa urahisi pasipo gherama kubwa na ambavyo huweza kupatikana au kuzalishwa shambani

Usalama kwa binadamu

Matumizi ya kemikali yanaweza kudhuru afya ya mlaji. Madhara yanaweza kutokea kutokana na kutohahamu maelezo ya matumizi. Aidha maelezo yanaweza kuandikwa kwa lugha isiyofahamika na mtumiaji. Matokeo yake madawa haya



Kutambua tatizo

Kabla ya kukabili magonjwa au wadudu ni vizuri kufahamu na kutambua tatizo lililopo. Unapofahamu na kutambua tatizo, unakua na uwezo wa kutibui aina ya madhara na vitu vinavyosababisha. Yanaweza kuwa ni ya hali ya hewa, upungufu wa madini au magonjwa yaliyosababishwa na wadudu. Kufahamu tatizo hupelekeea kukabili au kuzuia kwa ufanisi mkubwa zaidi.



Baadhi ya mbinu na njia za kiasili kukabili wadudu na magonjwa

Udongo wenye rutuba

Udongo uliohifadhiwa kwa mfumo hai huimarishe viwango vya rutuba. Mimea yenyne afya huweza kuhimili magonjwa na wadudu.

Mimea inayolishwa vizuri katika udongo mzuri hujikinga zaidi na hatari za wadudu na magonjwa

Madhumuni ya kutunza udongo ni

- Kuboresha rutuba (viumbe hai) katika udongo
- Lishe kwa viumbe walio kwenye udongo
- Kupatia mimea madini yanayofaa

Ijapokua kemikali huimarishe afya ya mmea, matumizi yake yamekuwa na madhara kadhaa. Mmea waweza kuwa na kiasi kikubwa cha naitrojeni itokanayo na kemikali na kuufanya uvutie wadudu. Imebainika kwamba wadudu hutaga mayai katika sehemeu zenye mimea iliyo na naitrojeni nydingi ukilinganisha na mimea iliypandwa kwa njia za kiasili



Haya ni magonjwa yanayoshambulia ng'ombe mara kwa mara na kusababisha hasara

Mimi ni msomaji wa jarida la MkM, napenda kuanzisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ila nimekuwa nikitatizwa na hofu ya magonjwa. Je naweza kufahamu baadhi ya magonjwa yanayoshambulia ng'ombe Mara kwa mara? -Haruni Melali-Arusha.

Margareth Mollel

Kuna magonjwa mengi sana yanayoshambulia ng'ombe na kusababisha madhara kiuchumi na kwa maendeleo ya sekta ya mifugo. Pamoja na hayo magonjwa mengi ya ng'ombe yanatibika kwa haraka endapo mfugaji atawahi.

Katika makala hii tutaainisha baadhi ya magonjwa yanayoshambulia ng'ombe mara kwa mara katika kanda mbalimbali.

1. Ugonjwa wa kimeta

- Ugonjwa huu husababishwa na bakteria.
- Bakteria hawa huishi ardhini kwa miaka mingi.
- Bakteria huingia mwilini mwa ng'ombe kupitia jeraha la puan na mdomoni.



Dalili za ugonjwa

- Uvimbere kwenye tumbo la uzazi na mafua ya uzazi.
- Kutoka mimba yenyenye umri wa miezi 5-8.
- Ng'ombe hushindwa kushika mimba.

Tiba na kuzuia



Angalizo

Mfugaji asithubutu kugusa nyama ya ng'ombe aliyeureka, kwani haifai kwa matumizi ya binadamu.

Tiba/kuzuia kimeta

- Kuchoma na kufukia mizoga yote ya ng'ombe waliokufa.
- Tandaza chokaa juu ya udongo na nyasi za kulalia juu ya shimo la futi

- Hakuna tiba muafaka ya ugonjwa.
- Chinja wanyama walioathirika ili kuzuia ugonjwa kuenea.
- Tenganisha wanyama waliotoka mimba na wazima kwa muda wa wiki 3.
- Chanja ndama wa miezi 3-9 mara kwa mara.
- Choma masalia ya vifaa vilivyonutika na wanayama walioathirika.

3. Ugonjwa wa miguu na midomo

- Chanja wanyama wote wazima kwa dawa inayopendekezwa na wataalamu.
- Wanyama wenye umri wa zaidi ya miezi sita wapatiwe chanjo kila mwaka kwa muda wa miaka 3 tangu mlipuko utokee.

Dalili za ugonjwa



- Ng'ombe hudhoofu kwa homa kwa muda wa siku 3-8.
- Uvimbere kwenye miguu na midomo ikiambatana na kutoka mate mengi.
- Mnyama kukosa uwezo wa kula kutokana na kuvimba midomo.
- Kupunguza uzalishaji wa maziwa.

Tiba



- Hakuna tiba rasmi lakini inashauriwa kuchanja.
- Tibu magonjwa nyemelezi

Kudhibiti na kuzuia

- Kupiga marufuku usafirishaji wa mifugo
- Kuwapatia chanjo wanyama wote ambaeo wapo katika eneo husika kwa usimamizi wa mtaalamu wa mifugo.

4. Kifua kikuu

Huu ni ugonjwa unaoathiri mifugo na binadamu.

Visababishi

Bakteria wa aina tatu ambaeo husababisha matezi ya mnyama kudhoofika, ingawaje huweza kushambulia maeneo yote ya mnyama.



Dalili za ugonjwa

- Uvimbere katika matezi ya mnyama.
- Dalili hubadilika kutegemeana na eneo la ugonjwa yaanikoo, mapafu, matiti au utumbo.
- Mnyama huanza kukohoaa mfululizo na kupoteza uzito

Kudhibiti na kuzuia

- Hakuna kinga wala tiba ya kisayansi kwa sasa, wala chanjo.
- Ondo wanyama walioathirika zizini.

5. Ugonjwa wa homa ya mapafu

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria kutoka kwenye kohozia na ng'ombe aliyeathirika

Dalili

- Joto kali.
- Kupumua kwa tabu.
- Kukohoaa mfululizo

6. Ugonjwa wa Ndorobo

- Husababishwa na vimelea wanaopatikana kwenye damu ya wanyama walioathirika.
- Mbung'o hueneza vimelea kutoka kwa ng'ombe mmoja hadi mwininge.



Dalili madhara

- Dalili hujitokeza siku 5-7 baada ya kueneza na mbung'o.
- Ng'ombe hypoteza nguvu, joto kali na hushindwa kula.
- Uvimbere kwenye tezi na mara nydingine kuharisha.

Tiba kudhibiti na kuzuia

- Kuna aina nyingi za dawa kwa ajili ya tiba kama vile Berenil, ethidium, novidium, na samorin.
- Epuka kuchunga ng'ombe kwenye misitu yenye mbung'o au karibu na wanyama pori
- Kuondoaa masalia ya mbung'o.
- Kuthibiti kuhamahama kwa mifugo

Ugonjwa wa homa ya bonde la ufa



Kumekuwepo na taarifa za matukio ya Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa(RVF) kaskazini mwa nchi ya Kenya na mashariki mwa nchi ya Rwanda kwa siku za hivi karibuni. Kwa mujibu wa taarifa za kiintelijensia za upashanaji wa habari (Veterinary Early Warning, Vyombo vya habari kutoka mamlaka ya hali ya hewa ya Kenya, Shirika la A fya ya Wanyama Duniani (OIE) na Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa(WHO) matukio haya yamesababisha watu kupoteza maisha na mifugo aina ya ng'ombe na ngamia kufa katika nchi jirani ya Kenya.

Fahamu maambukizi ya ugonjwa

Wanyama

Wanyama Kuumwa na mmbu au wadudu wengine wanaponyonya damu ya wanyama walioambukizwa virusi vya Homa ya Bonde la Ufa.

Binadamu

- Kuumwa na mmbu aliyeambukizwa.
- Kugusa damu au majimaji ya mnyama au binadamu aliyeambukizwa.
- Kula nyama isiyova vizuri.
- Kunywa maziwa ambayo hayajachemchwa.
- Kuchinja au kula nyama ya mnyama mgonjwa au mnyama aliyeuka.

Chukua tahadhari uonapo dalili zifuatazo Kwa wanyama

- Homa kali ambayo inaweza kuzidi nyuzi joto za sentigredi 41.
- Mnyama kuzubaa.
- Manyoya kusimama.
- Mimba kuharibika.
- Vifo vingi vya ndama au vitoto vya mbuzi na kondoo. Takribani 70% ya ndama katika kundi wanaweza kufa na kwa upande wa mbuzi na kondoo ni 95-100%. Kwa binadamu Homa kali, kuumwa kichwa, maumivu ya mwili, kizunguzungu, kichefuchefu, kutapika, kuharisha damu, kutokwa na damu mdomoni, puan, masikioni na kwenye ngozi, kupofuka macho na kupoteza fahamu.

Njia ya kuzuia maambukizi Kwa mifugo:

Kuogesha au kunyuniza mifugo kwa dawa za kuogesha mifugo, chanja mifugo ambaeo hawajaambukizwa na kuzika kwa tahadhari wanyama waliokufa.

Kwa binadamu

- Tumia chandaria chenye viuatilifi.
- Kuvalaa vifaa vya kinga:- glovu, koti na buti wakati wa kuchinja na kuchuna mmnyama.
- Kuepuka kula nyama ya mnyama mgonjwa au mnyama aliyeuka.
- Kuepuka nyama isiyovavizuri na maziwa yasiyochemshwa.
- Kusafisha kwa maji na sabuni visu na vyombo vinavyotumika kuandaa nyama.
- Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla na baada ya kuandaa nyama. Tahadhari kwa walaji wa nyama
- Kitoweo cha nyama iliyopikwa na kuiva vizuri ni salama.
- Zingatia tahadhari wakati wa kuchinja na kuandaa.
- Mishikaki isiyova vizuri inaweza kuwa chanjo cha uambukizo.
- Ni muhimu kutumia machinjio yaliyo rasmi.
- Hakikisha mifugo inakaguliwa kabla na baada ya kuchinjwa. Angalizo Ugonjwa wa homa ya bonde la ufa hautibiki hivyo zingatia tahadhari zilizotolewa ikiwi ni pamoja na kuhakikisha kwamba Ng'ombe, mbuzi na kondoo wanapata chanjo dhidi ya ugonjwa huu na uonapo dalili za ugonjwa huu toa taarifa kwa watoa huduma za afya mifugo.

Kwa maelezo Zaidi unaweza kuwasiliana na mtaalamu wa mifugo Prosper Linus kwa simu +255 756 663 247

Tengeneza dawa ya kutibu vidonda kwa kutumia gundi ya nyuki

Kwa ufugaji wa kisasa nyuki huvunwa mazao sita ambayo ni Asali (Honey), Nta (Bee Wax), Chavua (Pollen), Maziwa ya Nyuki (Royal Jelly), Sumu ya Nyuki (Bee Venom) na Gundi ya Nyuki (Propolis) ambayo leo tutajifunza namna ya kutumia kutengenezea dawa ya kutibu vidonda ijulikanayo kama Propolis Tincture.

Fredrick Katulanda

Gundi hii huvunwa kwa njia mbili. Mosi kwa kuweka kifaa cha kuvunia katika mzinga wako (*Propolis Trap*) au kuivuna kienyeji kwa kukwangua na kitu chenyencha kali katika mzinga maeneo ambayo nyuki wameiweka. Hata hivyo njia hii ya pili inapaswa kufanya kwa umakini ili kuepuka kuivuna na uchafu hivyo njia sahihi ni kuivuna kwa kifaa maalumu.



Picha:N

Nyuki anavyotengeneza gundi (propolis)

Ili kutambua gundi hii hupatikanaje kwa Nyuki, tunapaswa kujua kutoptana na nyuki kuwajibika kuitunza asali au kulinda makazi yao, Mungu amewajalia uwezo wa kuzalisha gundi kujilinda.

Katika mfumo wa maisha yao nyuki wanafanyakazi. Majike huhakikisha hakuna mdudu yoyote au kitu chochote kinaingia katika nyumba yao kuiharibu asali au kuwaua wao. Iwapo ikitokea kuwa kuna mdudu au kitu chochote kile, kimeingia kwenye



Picha:N

asali, basi nyuki watashirikiana kukishambulia kwa kudunga miba yao yenye sumu, lakini jithuda hiyo ikishindikana na kama adui mwenyewe ni mdogo basi watamtoa nje.

Lakini ikiwa kitu hicho au mdudu huyo ni mkubwa kiasi kwamba wao kwa uwezo wao wanashindwa kumtoa/kukitoa nje ya makazi yao, basi watatumia njia nyingine ya kuilinda asalina makazi yao. Kwa hatua hii watatengeneza ute maalumu (*Bee Resin*) na kuuchanganya na utomvu unaotokana na miti au baadhi ya mimea na ndipo hupata gundi ambayo inatambulika kama gundi ya Nyuki (*Propolis*). Hii huwasaidia kuzuia maadui aina yoyote ile wasiharibu asali au kuvamia makazi yao.

Baada ya kutengeneza gundi humzungushia mdudu au adui huyo

ute ambaao ni gundi ngumu yenye rangi nyekundu, bila ya kubakisha upenyo hata mmoja, kwa unene wa milimita moja na nusu (1.5mm) ili kumkinga asitoke hapo na kufanya uharibifu wowote katika makazi yao. Iwapo kama kwenye mzinga wao au makazi kutakuwa na nyufa ambazo zinaweza penyeza maadui, basi hutumia ute huo kuziba na unapokutana na hewa ya nje huganda mara moja na kuwa mgumu sana.

Hivyo kwa ufugaji wa kisasa *Propolis* huvunwa na kuuzwa kama bidhaa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutengeneza dawa ya kutibu vidonda ijulikanayo kama *Tincture*.



Picha:N

Jinsi ya kutengeneza dawa ya kutibu vidonda

Ili kutengeneza Dawa ya Kutibu Vidonda inakupasa kuwa na vifaa vifuatavyo;

- Chupa yenye mfuniko madhubuti na mdomo mpana.
- Gundi ya Nyuki kiasi cha grams 10.
- Spirit nyeupe kiasi cha ml 100.

Chukua gundi ya nyuki na kuiweka ndani ya chupa na kisha mimina Spirit ndani yake na kufunga na mfuniko wake na kuiweka sehemu ya kutulia yenye giza ikae kwa siku 21 na hakikisha unaitikisa vyema chupa hiyo mara mbili kila siku kwa siku zote ili kuifanya spirit ichanganyikane vyema na Gundi ya Nyuki.

Baada ya siku 21 fungua chupa yako kisha chuja dawa yako na kuhifadhi kwenye chupa kwa ajili ya kutumia kutibu vidonda hasa vipywa mara baada ya mtu kuumia.

Angalizo: Dawa hii isitumike kwa watu wenye matatizo ya kisukari bila idhini ya daktari.

Fuga nyuki kisasa kwa faida zaidi. Unaweza wasiliana na mtalaamu wa nyuki kwa Simu Na: +255 622 462620 kwa maelezo zaidi.



Picha:N

Je wajua Tangawizi ya Embe na faida zake katika mwili wa binadamu

Ni mmea wa familia ya tangawizi na inauhusiano wa karibu na manjano (*Curcuma longa*). Miti hii inafanana sana na tangawizi ya kawaida lakini haina ukali wake, na badala yake ina ladha ya embe mbichi. Ni moja ya mmea inayoheshimika katika mifumo ya dawa za asili huko Asia ya Kusini, Tangawizi ya embe inanyama thabiti, nyeupe na ya njano iliyokolea.

Stephano Aminiel

Tangawizi ya Embe inaota kwenye ardhi yenye unyevu na yenye rutuba, na lazima eneo liwe na kivili kidogo, na mwanga wa juu ni muhimu kwa ukuaji wake.

Faida za Tangawizi ya Embe

Tangawizi ya Maembe ni kiungo bora ambacho husaidia kutatta maswala mengi ya kiafya. Ingawa inaonekana kama tangawizi ya kawaida, ina ladha tamu ya embe mbichi. Kiungo hiki kwa kweli ni cha familia moja ya manjano, ina kiini cha manjano iliyokolea. Kulingana na tafiti, gramu 100 za viungo hivi hutoa gramu 10 za wanga, 25 miligramu ya kalsiamu, na 90 miligramu ya fosforasi.

Huimarishe afya ya mmeng'enywa wa chakula

Tangawizi ya Embe ina kimeng'enywa kinachoitwa enterokinase ambacho husaidia kuvunja protini kuwa ya kikaboni, ambayo husaidia usagaji wa chakula, na pia husaidia kuondoa gesi na kuongeza hamu ya kula.

Huboresha afya ya ngozi

Ina nguvu ya kemikali ambazo ni antioxidant na antimicrobial ambazo huondo sumu zote hatari mwilini, inasaidia kutibu matatizo tofauti ya ngozi kama chunusi na kuwashwa.

Hupunguza matatizo ya kupumua

Tangawizi ya Embe husaidia kupunguza makali ya ugonjwa wa pumu. Pia inatibu baridi katika mwili na kikohozi.

Husaidia kukabiliana na uvimbe

Tangawizi ya Embe inasaidia katika matibabu ya uvimbe kwenye viungo unaosababishwa na arthritis na rheumatism. Kulingana na wataalamu, mmea huu hutoa unafuu wa haraka kwenye uvimbe unaosababishwa na majeraha kama vili ya ajali.

Husaidia afya ya nywele

Tangawizi ya Embe inasaidia katika kuondoa mba kutoptana na sifa zake za kuzuia vijidudu na fangasi. Kupaka kibandiko cha Tangawizi ya Embe kwenye ngozi ya kichwa na nywele husaidia kuondoa mba na vipele kichwani.

Matumizi ya Tangawizi ya Embe katika upishi

Mara nyingi hutumiwa katika kachumbari, michuzi ikichanganya wa kama viungo vingine. Mtu anaweza kula mbichi pia pamoja na chumvi au akiichanganya na maji ya limao.

Unatayarishaje Tangawizi ya Embe

Wakati wa mavuno mapya yanapovunwa, andaa sehemu ya kuhifadhi tangawizi. Hakikisha



Picha:N

unaosha hizi vizuri na uzitumie kama viletangawizimbichiau manjano watu wengine huikuna, au kuiakatakata. Harufu mbichi ya embe na ladha ya tangawizi hufanya kachumbari, chai, au mchuzi kuwa na ladha nzuri. Tangawizi ya embe inaendana vizuri na tofu, kuku, dagaa, mboga za mizizi, na matunda ya kitropiki. Inapatikana pia kama poda iliyokaushwa, ambayo inaweza kutumika katika kupikia na maandalizi mengine ya nyama ya kuchoma.



Picha:N

Ni muhimu kuwa na njia mbalimbali za kuongeza kipato

Mkulima anapania kujihakikishia usalama wa chakula na kupata hela kutokana na shughuli zake za kilimo. Ikiwa, hauwezi kufanikisha malengo hayo, basi utakuwa unapoteza muda wako. Hivyo, ni vyema kujijengea tabia ya kuwa na shughuli mbalimbali zitakazokuwezesha kukabiliana na ushindani wa soko na pia kuiongezea kipato. Ukitegemea njia moja tu ya kipato, basi utakuwa unalemaza uwezo wako wa kuijina kiuchumi. Endapo njia hii moja itakuwa na changamoto basi utakuwa fukara haraka sana. Hii inahitaji ubunifu mkubwa.

Flora Laanyuni

Kuwa na shughuli mbalimbali ni moja ya mbinu muhimu inayotumiwa na wakulima vijijini katika kuiongezea kipato. Hii inaweza kuhusisha kukuza aina mbalimbali za mazao au kufuga aina tofauti za mifugo. Hapa, uwiano wa hatari unagawanya kwenye miradi mbalimbali kiasi kwamba, endapo soko halitakuwa zuri kwa bidhaa mojawapo, basi nyungine itachukua nafasi na hivyo anakuwa kwenye usalama, bila hasara kubwa. Hii inatumika zaidi kama njia ya kumuwezesha mkulima kuishi vizuri. Na, uwekezaji mpya kwenye miradi mbalimbali ni njia ambayo imeonesha kuwa na mafanikio.

Miradi mbalimbali

Ni lazima pia ielewewe wazi kuwa uanzishaji wa miradi mbalimbali unaweza kuwa changamoto kwa wakulima kwa kuzingatia upatikanaji wa mtaji wa kuanzisha. Uanzishaji wa mradi mpya shambani unahitaji pesa ambazo kwa wakulima walio wengi ni shida. Na hili limeendelea kubakia kuwa tatizo kwa wakulima wengi kufanya shughuli zao za kibashara nchini Tanzania.

Ili kupata mtaji, wakulima wanaweza kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa, taasisi za kifedha,



Picha:MKM

kupunguza gharama za pembejeo shambani na kujengea uwezo wa kupata masoko kwa ajili ya mazao yao ndani na nje ya nchi.

Tunaweza kusema kuwa uanzishaji wa miradi mbalimbali kwa wakulima wadogo wadogo ni jambo ambalo linahitaji mtaji kidogo, na hili linaweza kuleta unafuu kwa wakulima.

Miradi mbalimbali inasaidia kuimarisha kipato cha familia, na kutoa uhakika wa chakula, kiwe ni pamoa na uwezekano wa kupata chakula bora.

Tekeleza kilimo endelevu

Kufuata kanuni za kilimo endelevu, kama vile kutumia mbolea za asili na kupunguza matumizi ya viuatilifu, hakiwezi tu kunufaisha mazingira bali pia kuongeza kipato cha mkulima. Wateja wanazidi kuhamasika kuhusu umuhimu wa kula vyakula vilivyozaishwa kwa mbinu za kilimo hai na baadhi yao sasa wapo tayari kulipa bei ya juu kwa bidhaa mazingira ya mijini au maeneo mengine yasiyo ya kawaada. hivyo kupanua wigo wao wa soko.

Tumia teknolojia

Kuna njia nyngi ambazo wakulima wanaweza kutumia teknolojia ili kuongeza mapato yao. Kwa mfano, teknolojia za kilimo cha usahihi zinaweza kuwasaidia wakulima kusimamia mazao yao kwa ufanisi zaidi na kupunguza gharama. Umwagiliaji maji kwa matone humwezesha mkulima kuhifadhi maji na kuzalisha hata wakati wa kiangazi. Zaidi ya hayo, teknolojia mpya kama hydroponics zinaweza kuwawezesha wakulima kupanda mazao katika mazingira ya mijini au maeneo mengine yasiyo ya kawaada. hivyo

Shirikiana na wakulima wengine

Kila mara, jarida hili husizitiza ushirikiano kati ya wakulima. Kushirikiana na wakulima wengine, ama kupitia mipango ya ushirika inaweza kuwasaidia wakulima kkusanya rasilimali, kubadilishana maarifa, na kuongeza uwezo wao wa kusukuma na kutetea masilahi yao. Hii inaweza kuwasaidia wakulima kuongeza mapato yao kwa kupunguza gharama na kuboresha uwezo wao wa kuuza bidhaa zao.

Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana na Lucy Mvungi, Afisa Kilimo Halmashauri ya Arusha kwa namba 0755 565 621.

utalii wa kilimo kwenye mashamba yao, kama vile ziara za kielimu. Shughuli hizi zinaweza kutoa chanzo cha mapato kwa wakulima na pia zinaweza kusaidia kuongeza ufahamu na kuthamini kazi inayofanywa katika kuzalisha chakula. Watu wanapotembelea shamba lako, unawapa mafunzo na kuwatoza ada kidogo.

Kazi yangu inahusisha wakulima kwa sehemu kubwa, hivyo inanibidi nipite ofisi za Mkulima Mbunifu kuchukua nakala kadhaa za kufundishia wakulima. Nimejikita zaidi katika kilimo hifadhi nawafundisha wakulima kupanda mazao funika ili kuboresha afya ya udongo. Makala hio iliandikwa katika jarida la Mkulima Mbunifu kwa mapana.

Anasema kuwa jarida la Mkulima Mbunifu ni chaguo bora kwake na wakulima wengi kwa kutoa elimu muhimu kuhusu kilimo bora na njia

Bwana Shamba na mshirika wa Jarida la Mkulima Mbunifu

Jarida la Mkulima Mbunifu limeendelea kunufaisha jamii ya wakulima nchini Tanzania. Limejizolea umaarufu katika sekta ya kilimo kama jarida pekee la kilimo hai, Kwa jina lingine kilimo endelevu na pia unaweza liita jarida la kilimo ikilojia, kwani ni nyenzo ya ufundishaji kwa maafisa ugani, lakini pia limenufaisha wakulima moja kwa moja.

Erica Rugabandana

Kwa miaka iliyopita, yani 2022 kurudi nyuma jarida limechapishwa kila mwezi likisheheni Habari zinazolenga kilimo kinachoingatia afya ya mimea, afya ya mazingira, afya ya wanyama na hata human nutrition. Katika kipindi cha mradi 2023-2025 Jarida limekua likichapishwa mara moja kwa kila miezi miwili likitoa nafasi ya wahariri kutembelea wakulima na kupata taarifa zaidi za uzalishaji wenyi tija kwa mfumo wa kilimo hai.

Katika makala hii, tutaangazia Afisa ugani ambae, yeche amekua kinara wa kutumia jarida la mkulima Mbunifu. Huyu ni Bwana Bonaventure Charles (au Bonny) ambaye ni Afisa ugani katika shirika la ECHO Africa Mashariki. Yeye ni mtaalamu na kilimo hifadhi na maarufu katika kampeni ya kutokomeza gugu karoti ambalo limeathiri wanyama na binadamu.



Picha:MKM

mbadala za kilimo endelevu. Kupitia jarida hilo, amekuwa akipata taarifa mbalimbali kama tafiti na machapisho yenye kudumu kwa muda mrefu.

Hata hivyo, kupitia makala hii, kutokana na ufinyu wa maafisa ugani katika maeneo mengi Tanzania, anashauri wakulima walisake jarida hili kwani ni mbadala na linatoa taarifa mbalimbali kutoka wakulima wengine, watafiti na hata kutoka kwa maafisa ugani juu ya changamoto mbalimbali zinazokabili wakulima. Unaweza kujisajili ukapokea kila baada ya miezi miwili, au ukapata kwa njia za mitando na pia unaweza kuwapigia Mkulima Mbunifu wakakusaidia.

Hata ivyo aliongeza kuwa, mabwana shamba, maafisa ugani, wataalamu wa lishe, na wataalamu wa mifugo kuwa wabunifu katika kuchagua vyanzo vya elimu kama vile majarida ili kuwaelimisha watu na kufikia idadi kubwa ya wakulima.

Bonny anasisitiza kwamba Mkulima Mbunifu ni jukwaa muhimu kwa wakulima na wataalamu wa kilimo, na wanaweza kunufaika sana kutokana na machapisho yake yanayodumu kwa muda mrefu.

Anasisitiza kuwa jarida la Mkulima Mbunifu ni jukwaa muhimu kwa wataalamu wa kilimo na wanapaswa kutumia vyanzo kama hivyo kuelimisha watu na kufikia idadi kubwa ya wakulima.

Kwa Bonny, jarida la Mkulima Mbunifu si tu chanzo cha elimu bali ni mwongozo wa kubadilisha kilimo nchini Tanzania.

Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana na Bonaventure Charles kwa simu namba 0754992079 Arusha



Picha:MKM



Picha:MKM

Sikiliza vipindi vya kilimo ikolojia

Kama ilivyo ada *Mkulima Mbunifu* imeendelea kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha inakufikishia taarifa sahihi za kilimo hai. Kwa mantiki hiyo, usiache kusikiliza vipindi vya kilimo hai vinavyoletwa kwako na shirika la Farm Radio International kupitia stesheni mbalimbali za radio.



JINA LA RADIO	JINA LA KIPINDI	NAMBA YA KUBIPU	SIKU YA KIPINDI		MARUDIO YA KIPINDI	
			SIKU	MUDA	SIKU	MUDA
RADIO MWANGAZA	KILIMO NA MWANGAZA	784105727	IJUMAA	2:30-3:00 USIKU	JUMATATU	2:30-3:00 USIKU
RADIO STANDARD FM	KILIMO NA JAMII	784105733	JUMAMOSI	1:00-1:30 JIONI	JUMATANO	1:30-2:00 USIKU
RADIO UTUME	KILIMO NA MKULIMA	784105788	ALHAMISI	2:30-3:00 USIKU	JUMAPILI	1:00-1:30 JIONI
RADIO HABARI NIJEMA	JUKWAA LA MKULIMA	784105711	JUMAMOSI	3:00-3:30 USIKU	JUMATANO	3:00-3:30 USIKU
RADIO SAUTI YA INJILI	JICHO LA MKULIMA	784105718	JUMAMOSI	1:30-2:00 USIKU	JUMATANO	12:00-12:30 JIONI

Je, wafugaji wa kuku wanamaswali gani?

Mshindi anasema; Asante kwa elimu mnayoitoa kwetu, Nimesoma kuhusu uchanganyaji wa chakula cha kuku na mmeonyesha kuwa unaweka mahindi kwa kila rika, ila sijaona mahali mlipoonyesha kuhusu vifaranga wa siku 1 na kuendelea. Je, unachanganyaje chakula chao maana wale wanahitaji chakula kilichosagwa?

Mkulima Mbunifu: Habari, karibu *Mkulima Mbunifu* na asante kwa kuendelea kusoma na kufuatilia Makala mbalimbali za jarida hili. Kwa vifaranga wa siku moja mpaka miezi miwili unahitajika kuchanganya chakula chao kama ifuatavyo;

- Unga wa dona wa mahindi au mtama kg 40
- Pumba za mtama, mahindi au uwele kg 27

- Mashudu ya alizeti, ufuta, pamba au karanga kg 20
- Unga wa mifupa au chokaa ya kuku kg 2.25
- Dagaa au mabaki ya samaki kg 10
- Chumvi 0.5
- Premix 0.25
Jumla utapata kilo 100 na utalisha kulingana na wingi wa vifaranga wako.

kijulikanacho kama trypsin hivyo mashudu ya soya ndiyo hutumika na siyo maharage yenewe.

Isah Mahila anauliza: Je, kuna uhusiano wa lishe husika na jamii ya kuku wa kienyeji? Yaani kama ni kuchi atakula chakula tofauti na aina nyingine ya kuku?

Mkulima Mbunifu: Habari, karibu *Mkulima Mbunifu* na asante kwa swali lako. Hakuna tofauti kwenye lishe kwa kuku wa kienyeji aina yeoyote isipokuwa lishe huwa tofauti baina ya vifaranga na kuku wakubwa na hasa kwa vipimo na uandaaji wa chakula husika.

Kwa maswali zaidi ya ufugaji kuku wasiliana na mtaalamu wetu Eliudi Letungaa kwa simu namba +255764266527.

Je, wajua sababu kumi za kuendeleza kilimo hai

- Chakula kinakuwa na ladha ya asili: ladha yake ni nzuri
- Kimesheheni viinilishe vya asili vya kutosha kwa afya: kwa asili kinajenga afya.
- Hakina mabaki hararishi ya kemikali: hakina kemikali
- Kinaepusha matumizi ya vyakula viliwyobadilishwa vinasaba / gmo: kinatunza afya ya mlaji
- Havisababishi magonjwa yanayosababishwa na upulizaji wa kemikali kwa mkulima wala mlaji: mkulima na mtumiaji/ mlaji hubakia salama
- Kinahimiza utunzaji wa bioanuai na mbegu za asili: mbegu zisizowekewa hataza
- Kinachangia kuboresha afya ya udongo, mimea na wanyama: ni mwafaka wa kwa mazingira ya asili
- Kinatambua maasifa asili ya mkulima : kinaheshimu busara za asili
- Kinashabihiana na kilimo endelevu pamoja na njia za uzalishaji chakula: uendelevu wa uhakika wa chakula
- Hakichafui na kuharibu mazingira: ni rafiki wa mazingira



Picha:N



mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagram.com/mkulima_mbunifu

